TANGAZO LA SERIKALI NA. 438 la Tarehe 31/5/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 16 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO, 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ya Mwaka 2024, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ya Mwaka 2023 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

TS Na. 918 la 2023

Marekebisho ya aya ya 3

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika tafsiri ya maneno "Mkurugenzi" kwa kufuta neno "Biharamulo" yaliyo katika aya ya 3 na badala yake kuweka neno "Kibondo".

Marekebisho ya aya ya 7

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 7 kwa kufuta aya ndogo ya (5).

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

4. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza Sehemu ya Tatu kipengele cha 8 kwa kufuta maneno "kwa siku" yaliyo baada ya tarakimu 25,000/= na badala yake kuweka maneno "kwa tukio".

Dodoma,
18 Aprili, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa)*